CHUO KIKUU CHA TEKNOLOJIA
CHA DEDAN KIMATHI

HATI YA UTOAJI
HUDUMA KWA WATEJA

DeKUT is ISO 9001:2008 Certified

"Maisha Bora Kupitia Teknolojia"

UJUMBE KUTOKA KWA MWENYEKITI WA BARAZA LA CHUO KIKUU CHA TEKNOLOJIA CHA DEDAN KIMATHI

Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Dedan Kimathi ni Chuo ambacho kina nguzo tatu kuu ambazo zinakiwezesha kutekeleza majukumu yake ambayo ni elimu ya kiwango cha juu,ubora wa utafiti na huduma kwa jamii.Hati ya utoaji huduma ya Chuo hiki inalenga kutekeleza wajibu huu.

Hati hii inatarajia kuelimisha umma kuhusu huduma ambazo Chuo hiki kikuu kinatoa. Kwa hakika,hii ni haki ya kijamii baina ya Chuo hiki na washika dau wake. Vile vile itatuwezesha kutathmini ubora wa huduma zetu. Imerahisishwa ili kumwezesha mteja wetu yeyote kumrejelea kwa muda mchache na kupata afisa au idara inayohusika na huduma anayohitaji. Tunatambua jukumu letu la kutekeleza huduma iliyo katika hati hii.

Hati hii inazingatia maoni muhimu kutoka kwa wasimamizi wa Chuo hiki na washika dau mbali mbali.

Nikiwa mwenye kiti wa Baraza la Chuo hiki, ningependa kusisitiza jukumu letu la kutoa elimu bora ya kiteknolojia kwa vile ni nyenzo kuu katika kukuza uchumi kote duniani. Tunalenga kuwawezesha wahitimu kuwa na maarifa ambayo yanahitajika katika ajira hapa nchini na kimataifa.

Profesa Dulacha B. Galgalo

Mwenyekiti

UTANGULIZI

Hiki Chuo Kikuu ni taasisi ya elimu ambayo inatoa mafunzo ya kiwango cha juu na utafiti unaoambatana na malengo ya nchi yetu katika mpango wa Vision 2030. Mamlaka yake ni kukuza wafanyikazi ambao watachangia maendeleo ya kiuchumi, kitamaduni, kijammii, kiteknolojia na kisanyansi katika nchi yetu. Hii hati inaashiria kujitolea kwetu kiumarisha huduma zetu na mawasiliano kati yetu nawe. Hati hii pia ni azimio wazi kwa wateja ili kudhihirisha dhamira yetu kwa huduma bora, uenda kazi na ufanisi wetu.

Ni matarajio yetu kuwa hati hii itaboresha huduma na kuwa chombo cha kukuza maadili kazini, ufanisi na kuridhisha.
Tunapozindua hii hati, tunawahimiza wafanyikazi wote kuzingatia ahadi zetu na kufanya kazi kwa pamoja kazini. Tuna majukumu ya kutekeleza na uwajibikaji katika vitendo vyetu.



Profesa Mhandisi P. Ndirangu Kioni

Mkuu wa Chuo, DeKUT

Madhumuni ya Hati ya Utoaji Huduma

Madhumuni ya hii hati ni kuwaelimisha wateja wetu kuhusu huduma za DeKUT. Inaweka viwango ambavyo utakavyotarajia kutoka kwetu na niazimio letu kwa umma linalolenga wateja kuhusu dhamira yetu ya huduma bora na ufanisi katika utenda kazi.
Inatoa maelezo kuhusu jinsi unavyoweza kupata habari na vile ambavyo unaweza kuwasiliana nasi ikiwa una maoni.
Fadhila mahususi ya hati hii ni ahadi yetu kuzingatia maadili ya kitaaluma na huduma bora.

Wito

Maisha bora kupitia teknolojia

Maono

Kuwa Chuo Kikuu cha Teknolojia chenye hadhi ya juu na kiwango cha juu cha elimu, utafiti na uenezi wa teknolojia kwa madhumini ya kuhamasisha maendeleo ya taifa.

Jukumu

Kutoa mazingira bora ya kielimu yanayodhihisha tamaduni mbalimbali yanoyojumuisha utafiti,, ubunifu na maendeleo ya kiteknolojia ili kuzalisha wafanyikazi na viongozi watakaochangia katika malengo ya maendeleo ya kitaifa.

Falsafa ya Chuo Kikuu cha Teknologia cha Dedan Kimathi

Chuo kuku cha Teknologia cha Dedan Kimathi kimejengwa juu ya imani kwamba kujiaamini kwa mtu and ufumbuzi wa changamoto zinazo kumba dunia waweza patikana kupitia roho ya kujitolea, kujiamini, kutokata tamaa, na matumizi mazuri ya rasilimali. Chuo

hiki kinaamini kuwa chuo cha hadhi ya juu duniani kupitia uwezo unaotambulika kimataifa. Ili kuwezesha imani na malengo yake, chuo hiki kinanuia kuwekeza katika wafanyikazi wake, majumba na vifaa vya kufunza na mifumo ili kuhakikisha mazingira mema yanayotambulika kimataifa yanapatikana kwa madhumuni ya masomo na kuendeza malengo yake.
Lengo la juu la falsafa hii ni kukifanya Chuo Kikuu cha Teknologia cha Dedan Kimathi kuwa chuo kunachojulikana kwa utafiti unaoenziwa kimataifa, masomo ya hadhi ya juu, wanafunzi bora, na kuwa na kiwango cha juu kabisa cha uvumbuzi, ubunifu, usomi na bishara.

Maadili Makuu ya chuo kikuu cha Teknolojia cha Dedan Kimathi

Maadili makuu yanajumuisha imani za kimsingi zinazoongoza chuo hiki. Katika kutimiza jukumu lake, chuo hiki kitaongozwa na maadili yafuatayo makuu:-

- Ubunifu
- Usomi
- Uanuwai
- Uadilifu
- Umoja

MKATABA WA UTOAJI HUDUMA

Kujitolea kwetu katika utoaji huduma

NA MBA	HUDUMA	JUKUMU	ADA	MUDA	IDARA HUSIKA
1	Maswali	Kuzuru chuo	Haipo	Dakika kumi na tano (15)	Idara zote
2	Maswali	kupiga simu	Haipo	Dakika kumi (10)	Huduma ya Wateja
3	Wanafunzi na wananchi waweze kuzuru afisi	Maafisa kuwahudumia wanafunzi na wananchi	Haipo	Afisi zote hufunguliwa kati ya saa mbili asubuhi na saa kumi na moja jioni	Wafanyi kazi wote
4	Utoaji barua za kusajiliwa	Maafisa katika afisi ya msajili (maswala ya Akademia) kutayarisha vyeti na hati za matokeo ya mtihani	Haipo	Tunakubali maombi katika muda wa siku saba (7)	Msajili (maswala ya akademia)
5	Vyeti vya chuo na hati za matokeo ya mtihani	Afisi ya msajili (maswala ya Akademia) kutayarisha vyeti na hati za matokeo ya mtihani	Haipo	Vyeti vitatolewa katika muda wa mwezi mmoja (1) baada ya kufuzu	Msajili (maswala ya Akademia)
6	Ununuzi wa bidhaa na huduma za umma	Kufuata mchakato wa ununuzi wa bidhaa na huduma za umma	Haipo	Kufanyika katika muda wa siku sitini (60)	Afisa wa ununuzi wa bidhaa na huduma za umma

7	Upishi na malazi	Chuo kuwafahamisha wanafunzi kuhusu huduma za upishi na malazi	Haipo	Taarifa kutolewa katika muda wa majuma mawili (2) kabla ya mwanzo wa muhula	Mpishi mkuu na msimamizi wa maswala ya usafi
8	Malipo kwa watoaji bidhaa na huduma	Uwasilishaji bidhaa na huduma	Haipo	Malipo katika muda wa siku sitini (60)	Afisa mkuu wa fedha
9	Matokeo ya mtihani ya muhula	Wanafunzi kufanya mtihani	Haipo	Matokeo kutolewa katika muda wa miezi miwili (2) baada ya mitihani kukamilika	Wenye kiti wa idara
10	Uhamisho baina ya vyuo vikuu	Kuidhinishwa na kamati ya wakuu wa vyuo	Haipo	Muda wa wiki mbili (2) baada ya kufungua chuo	Msajili (maswala ya akademia)
11	Kuandikisha wanafunzi	Kufuata mchakato wa kuandikisha wanafunzi	Haipo	Muda wa wiki mbili (2) baada ya kufungua chuo	Msajili (maswala ya akademia)
12	Malalamishi kuhusu huduma	Kuwasilisha malalamishi rasmi	Haipo	Siku kumi na nne (14) baada ya kupokea malalamishi	Kamati ya malalamishi

* Kwa kuwa kila idara inatoa huduma za asili ya kipekee kuna mikataba ya huduma katika kila idara ambayo inaonyesha jinsi na wakati ambapo huduma zitapeanwa sanjari na dira na dhamira ya mkataba huu.

Malalamishi yanafaa kuwasilishwa kwa wakuu wa idara na iwapo utakumbana na tatizo lolote katika kupata huduma kutoka kwa idara yoyote, tafadhali, tuma malalamishi kwa:

Mkuu wa Chuo- 0736 456391;
Barua Pepe: vc@dkut.ac.ke AU

Katibu- Kamati la Malalamishi- Barua Pepe:
complaints@dkut.ac.ke AU

Mwenyekiti Baraza la DeKUT- Barua Pepe:
councilchair@dkut.ac.ke AU

Tume la Haki Tawala
SLP 20414, 00200-Nairobi
Simu: 0710 936000
Barua Pepe: info@ombudsman.go.ke
Tovuti: www.ombudsman.go.ke

Jukumu Letu

Kubuni na kutekeleza mtaala ambao unatimiza mahitaji ya viwanda, kufanya utafiti na ushauri na kuhimiza ushirikiano na washika dau mbali mbali.

Majukumu ya Kimsingi

Kutoa elimu ya kiwango cha Chuo kikuu, mafunzo bora, utafiti na kuhusika katika kubuni, kupokeza na kukuza maarifa:-

- Kutoa elimu ya kitaaluma ambayo ni bunifu, mwafaka na inayotosheleza mahitaji ya soko katika viwango vya kwanza na zile za uzamili na uzamilifu zenye mfumo wa ubora ambao unajitegemea.
- Kutathmini na kupendekeza muundo msingi mpya, shule, taasisi, idara, vituo vya utafiti, shahada na taaluma mpya za elimu.
- Kushiriki katika mipango ya jamii na shughuli ambazo zinahusisha ushauri kama mojawapo majukumu ya kimsingi.

(a) Jukumu kuu la chuo kikuu litakuwa:

(i) Kufunza wanafunzi, kushirikiana na vyuo na mashirika mengine ilikuleta uwiano wa masomo, utafiti, and utumizi mwema wa maarifa na ujuzi kwa maisha, kazi na ustawi wa raia wa Kenya.

(ii) Kushiriki katika kazi ya kitaalamu, ugunduzi, uenezi, matumizi, utunzaji na uimarishaji wa maarifa na kuhimiza ushiriki wa kiakili wa wanafunzi katika maendeleo ya Kenya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kisayansi na kiteknolojia.

(iii) Kutoa kozi endelezi za maendeleo ya kitaaluma.

(iv) Kuamua mitaala na mfumo wake wa utoaji na kutoa vigezo vya kusajiliwa kama mwanafunzi.

(v) Kutoa mitihani na kutoa tuzo za kitaaluma kulingana na Sheria na Katiba ya Chuo.

(vi) Kuanzisha vyuo vipya, vyuo vya kozi, shule, taasisi, idara, na vitengo na vituo vya kiutawala na na kusimamia rasilimali nyingine.

(vii) kukuza vyema ustawi wa jumla wa wafanyakazi na wanafunzi.

(b) Kusajiliwa kama mwanafunzi katika Chuo Kikuu au kuteuliwa kama mfanyikazi na uendelezaji wa wafanyakazi utakuwa wazi kwa watu wote bila ubaguzi wa rangi, kabila, pahali asili, makaazi au uhusiano nyingine za mitaa, uwezo wa kiuchumi na kijamii, rangi, imani, uwezo wa kimwili au jinsia; ujauzito, hali ya ndoa, dini, dhamiri, imani, utamaduni, mavazi, lugha au kuzaliwa.

Malengo Yetu ya Kimkakati

1. Kuanzisha mtaala wa elimu teknolojia ya Chuo kikuu ambayo ni kiwango cha juu mwafaka inayopatikana kwa urahisi.
2. Kupanua shughuli zetu za ushirikiano wetu na viwanda, jamii, mashirika ya kimataifa na taasisi za mafunzo na utafiti.
3. Kukuza uwezo wetu wa kuhimiza utafiti na ubunifu.
4. Kusambaza teknolojia na kuendeleza biashara inayotokana na ubunifu.


Madhumuni Yetu ya Kimkakati

1. kutoa wahitimu bora sambamba na mamlaka ya chuo hiki.
2. kutoa utafiti na matokeo bunifu na saidizi kwa malengo ya maendeleo ya taifa.
3. Kueneza teknolgia kutoka Chuo Kikuu na taasisi zingine za kimataifa na kuifanya biashara kwa manufaa ya wanafunzi, Chuo Kikuu na sekta ya viwanda.

Mfumo na Usimamizi

DeKUT ni Chuo Kikuu ambacho kilibuniwa na sheria ya KUCT Act Nambari 162 ya mwaka wa 2007.

- Kansala ndiye anayefanya majukumu kwa kuzingatia Sheria za Chuo Kikuu.
- Baraza la Chuo kikuu ndilo lenye mamlaka makuu ambalo limepewa jukumu la kuendesha shughuli za Chuo na usimamizi wake.
- Mkuu wa Chuo ndio msimamizi wa maswala ya kitaaluma na utenda kazi Chuoni na afisa mwajibikaji.
- Naibu wa mkuu wa Chuo (A&F) ndiye msimamizi wa utenda kazi na fedha pamoja na wafanyakazi.
- Naibu wa mkuu wa Chuo (AA) ndiye msimamizi wa masomo katika Chuo.
- Naibu wa mkuu wa Chuo (RTMCL) ndiye msimamizi wa utafiti na wahadhiri katika Chuo.
- Bodi ya halmashauri (Seneti) huendesha shughuli zote za mafunzo katika Chuo kikuu.



Kielelezo 1: Muundo wa Uongozi

Wateja Wetu

Wafuatao ndio wateja wa Chuo hiki miongoni mwa wengine:-

- Wanafunzi
- Wafanyikazi
- Wazazi/ walezi
- Wahuduma
- Wanafunzi wa zamani walio fuzu
- Jamii
- Taasisi zingine
- Umma

Washirika na Washika Dau Wetu

Wafuatao ndio wabia wetu miongoni mwa wengine:-

- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MOHEST)
- Bodi ya Mikopo kwa Masomo ya Juu(HELB)
- Tume la Masomo ya Chuo Kukuu (CUE)
- Chuo Kukuu cha Teknologia na Kilimo cha Jomo Kenyatta
- Vyuo vikuu vingine
- Idara za serikali
- Watafiti
- Washirika wa kibiashara na viwanda
- Wahisani na wadhamini
- KENET na washiriki
- Muungano wa wanafunzi na majirani
- Mashirika ya kitaaluma na washika dau wengine

Ahadi Yetu kwa Wateja

DeKUT inaahidi:-

- Kuwaheshimu wateja wote bila kumbagua yeyote.
- Kuwepo kwa uwazi katika usajili.
- Kutoa huduma bora zenye ufanisi.
- Kuhakikisha kuwepo kwa nidhamu Chuoni.
- Kuchapisha vigezo na viwango vya kutathmini utenda

kazi mara kwa mara na kuchapisha moteko kulingana na viwango hivyo.
- Kubuni vituo vya mawasiliano kuhusu maswala na kutatua migogoro.
- Kufuatilia na kuhakikisha jinsi unavyoridhika na huduma yetu na kuiboresha mara kwa mara ili kukidhi mahitaji yako.

Majukumu ya Wateja wa DeKUT

Wateja wetu wanatarajiwa kuzingatia yafuatayo:-

- Kujifahamisha kuhusu sera zetu za kitaaluma na jukumu kuu la Chuo kikuu.
- Kuhudhuria mipango yote iliyoratibiwa.
- Kuzingatia kanuni na sera za serikali.
- Kutoa habari sahihi, uaminifu na kwa wakati ufao ili tuweze kukuhudumia vyema.
- Kutoa maoni na mapendekezo yanayoeleweka kupitia kwa anawani yetu na kisanduku cha maoni.

Marejeleo ya Hati Hii

Mabadiliko katika Hati hii ya utoaji huduma yatafanywa yanapohitajika baada ya ushuriano kati ya Chuo na wateja wetu miongoni mwa washika dau wengine ili kuboresha huduma na ufanisi wa majukumu yetu.

Maoni na Marekebisho

Tumejitolea kudumisha heshima na kuboresha huduma. Hata hivyo, wateja wetu ambao watakosa kupata huduma yetu au kupokea huduma duni kulingana na vigezo vyetu, wawasiliane nasi kwa anwani zetu ambazo zimetolewa hapo chini ili tutatue malalamiko yao.

Utatuzi wa Malalamiko

- Wateja wetu wanahimizwa kuwasilisha malalamiko au maoni yao kwa wakuu wa idara husika na ikiwa ni rufaa kwa afisi ya Mkuu wa Chuo kikuu.
- Chuo kikuu kinaahidi kuweka vijisanduku vya maoni katika sehemu zinazofaa ili kupokea maoni
- Chuo kikuu kitashughulikia malalamiko katika kipindi cha siku kumi na nne (14).

Mkuu wa Chuo Kikuu,
Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Dedan Kimathi
SLP 657-10100, Nyeri
Simu 061-2050000
Barua pepe: vc@dkut.ac.ke
Tovuti: www.dkut.ac.ke

.....

Tume la Haki Tawala
SLP 20414, 00200-Nairobi
Simu: 0710936000
Barua pepe: info@ombudsman.go.ke
Tovuti: www.ombudsman.go.ke

TAARIFA YA DEKUT KUHUSU SERA YA UBORA

Usimamizi na wafanyikazi wa DeKUT wana dhamira ya kutoa elimu bora na nafuu, utafiti wa kiwango cha juu, huduma bora na sahihi kwa wateja wake sasa na wanaotarajiwa kwa wakati unaofaa na kuridhisha wateja kutokana na kuwepo nia baina ya wasimamizi wakuu wa Chuo, ufanisi wa uongozi, kazi ya pamoja na usimamizi mwema wa wafanyikazi wote.

DeKUT kitawaridhisha wateja kuendelea kuimarisha michakato, bidhaa na huduma ili kukidhi au kuzidi mahitaji ya wateja.

Ili kutekeleza nia hii, DeKUT imeweka mfumo wa viwango ambao unaambatana na vigezo vya ISO 9001: 2008 vya kimataifa na kanuni mbali mbali za serikali zinazozingatiwa na wafanyikazi wote na tutaendelea kuimarisha ufanisi katika ubora wa mifumo ya usimamizi na malengo yake kupitia marejeleo ya mifumo hiyo mara kwa mara kulingana na viwango mwafaka vya ubora.

Sahihi .....

Tarehe .....

Profesa Mhandisi P. Ndirangu Kioni

Mkuu wa Chuo, DeKUT



TOVUTI:

www.dkut.ac.ke